

## Huduma ya Ushauri wa Kitaalamu Kiafya ya Mkoa Mzima

*Huduma inayotolewa na Kituo cha Afya ya Akili cha Queensland kwa Tamaduni mbalimbali.*

### Karatsi ya Habari kwa Watumiaji (Swahili)

Umekutana na Mshauri wa Afya ya Akili wa Lugha Yako (BMHC) kutoka Kituo cha Huduma ya Afya ya Akili ya Tamaduni Mbalimbali cha Queensland (QTMHC).

Jina la Mshauri wa Afya ya Akili wa Lugha Yako ni: \_\_\_\_\_

QTMHC inatoa huduma kupita Washauri wa Afya ya Akili wa Lugha Yako:

- Tathmini sahihi ya Kitamaduni
- Ufafanuzi wa masuala ya kitamaduni yanazohusiana na suala la afya ya akili yako
- Msaada katika maendeleo au mapitio ya mpango wa malezi yako binafsi
- Msaada wa muda mfupi, kama vile taarifa na elimu kuhusu suala la afya yako ya akili wewe na mlezi wako.

#### Haki zako

Una haki ya:

- kufanya maamuzi kuhusu afya yako
- kupokea msaada wa kitaalamu bila ubaguzi kwakuzingatia utamaduni wako, umri, hadhi ya kijamii, jinsia, upendeleo mapenzi, dini au imani ya kisiasa
- Kuweza kuelezewa kuhusu hali yako, ugonjwa na mipango kwa ajili ya usimamizi ambao unaweza kuuelewa
- Kuweza kuheshimiwa kwa usiri wako
- kuomba, na kupewa mkalimani kama inatakiwa

- Kuwa na mtu kukusiadia (rafiki, jamaa, mfanyakazi) kushiriki katika masuala yote ya huduma yako
- kufanya malalamiko kuhusu dhana yoyote ya huduma yako kama haujaridhika.

#### Wajibu wako

Unatiwa moyo kufanya kazi na wataalamu wa afya ya akili ili uweze kutunza afya yako mwenyewe kwa:

- kujibu maswali kuhusu afya yako kwa uwazi iwezekanavyo
- kutunza miadi yako na kuruhusu mfanyakazi wa afya yako kujua kama wewe unaweza kuhudhuria miadi yako
- kufuatia tiba au usimamizi ambao umekubaliana nao na kuwaambia wafanyakazi wako wa afya kama ukiamua kutoendelea na matibabu yako
- kuruhusu mfanyakazi wa afya yako kujua kama wewe unaonana na wahudumu wengine wa afya kuhusu tatizo hilo hilo.

Kama unahitaji maelezo zaidi, ungependa kujadili matatizo yako, au kufanya malalamiko, unaweza piga (07) 3167 8333 (katika Brisbane) au 1800 188 189 (nje ya Brisbane), na kuuliza kuzungumza na Mratibu wa Huduma ya Utalaamu au Meneja.

Kama huna hauzungumzi Kiingereza, tafadhali piga simu kwa 131450 kuomba mkalimani katika lugha yako na uliza kuunganishwa na Kituo cha Afya ya Akili cha Queensland kwa (07) 3167 8333. Gharama ya mkalimani hulipwa na Kituo.